JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

BUNGE LA TANZANIA

# ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

## MKUTANO WA KUMI

## KIKAO CHA KWANZA

30 JANUARI, 2018

# ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

---

## MKUTANO WA KUMI

## KIKAO CHA KWANZA – TAREHE 30 JANUARI, 2018

**I. WIMBO WA TAIFA:**

**II. DUA KUSOMWA NA KIKAO KUANZA SAA TATU ASUBUHI:**

**III. KIAPO CHA UAMINIFU:**

1. Mhe. Dkt. Damas Daniel Ndumbaro
2. Mhe. Justin Joseph Monko
3. Mhe. Dkt. Stephen Lemomo Kisurwa

**IV. TAARIFA YA SPIKA:**

## V. HATI ZA KUWASILISHA MEZANI:

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:**

Maelezo ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali kuhusu Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali (Na. 5) wa Mwaka 2017 *[The Written Laws (Miscellaneous Amendments) (No. 5) Bill, 2017].*

**MWENYEKITI WA KAMATI YA KATIBA NA SHERIA:**

Maoni ya Kamati ya Bunge ya Katiba na Sheria kuhusu Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali (Na. 5) wa Mwaka 2017 *[The Written Laws (Miscellaneous Amendments) (No. 5) Bill, 2017].*

**MSEMAJI MKUU WA KAMBI RASMI YA UPINZANI KUHUSU WIZARA YA KATIBA NA SHERIA:**

Maoni ya Msemaji Mkuu wa Kambi Rasmi ya Upinzani kuhusu Wizara ya Katiba na Sheria juu ya Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali (Na. 5) wa Mwaka 2017 *[The Written Laws (Miscellaneous Amendments) (No. 5) Bill, 2017].*

## VI. MASWALI:

### OFISI YA WAZIRI MKUU:

**1. MHESHIMIWA IBRAHIM MOHAMEDALI RAZA (KIEMBE SAMAKI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri Mkuu:-

Je, ni lini Serikali itachukua hatua ya kuwasaidia Vijana walioathirika na matumizi ya Dawa za kulevya.

**2. MHESHIMIWA SALUM MWINYI REHANI (UZINI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri Mkuu:-

Je, ni lini Serikali itawatambua rasmi madereva wa bodaboda na bajaji kwa kuwaandikia Mikataba, kuwawekea akiba na kulipiwa Mifuko ya Hifadhi ya Jamii na waajiri wao kwani vijana hawa wameshajiajiri kwa zaidi ya asilimia 15 - 25 kwenye kila Wilaya au Halmashauri.

## OFISI YA RAIS (TAMISEMI):

**3. MHESHIMIWA ENG. EDWIN AMANDUS NGONYANI (NAMTUMBO):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):- Wilaya ya Namtumbo haina huduma stahiki za Hospitali ya Wilaya wala Vituo vya Afya licha ya kuwepo kwa Sera ya kila Wilaya iwe na Hospitali ya Wilaya na kila Kata iwe na Kituo cha Afya:-

(a) Je, Sera hiyo kwa Wilaya ya Namtumbo itatekelezwa lini;

(b) Makadirio yaliyofanywa na TBA kwa ujenzi wa Hospitali ya Wilaya ya Namtumbo ni Tsh. 19 bilioni. Je, Serikali ipo tayari kutenga na kutoa kiasi hicho katika bajeti ya mwaka 2018/2019;

(c) Je, Serikali ina mpango gani wa kutoa vitendea kazi na wataalam katika Vituo vya Afya vitano vilivyopo Namtumbo ili viweze kutoa huduma bora za afya.

4. **MHESHIMIWA LOLESIA JEREMIAH BUKWIMBA (BUSANDA):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):- Tatizo la uhaba wa Watumishi katika Sekta ya Afya kwenye Halmashauri ya Wilaya ya Geita ni kubwa sana:-

Je, Serikali ina mkakati gani wa dharura wa kuliondoa tatizo hilo.

5. **MHESHIMIWA REHEMA JUMA MIGILLA (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):-

Je, ni lini Serikali itaondoa vikwazo kandamizi kwa Walimu wanaotaka kuhama vituo vyao vya kazi kwa hiari yao kutokana na sababu mbalimbali.

6. **MHESHIMIWA MWITA MWIKWABE WAITARA (UKONGA):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano:- Katika Mtaa wa Mongolandege Kata ya Ukonga kuna Daraja la Mongolandege ambalo huunganisha Jimbo la Ukonga na Jimbo la Segerea. Aidha, Daraja la Mto

Nyeburu huunganisha Kata ya Buyuni na Kata ya Chanika Magengeni:-

Je, ni lini Serikali itajenga Madaraja hayo muhimu ili kurahisisha huduma za kijamii katika maeneo yaliyotajwa.

## WIZARA YA FEDHA NA MIPANGO:

**7. MHESHIMIWA SALMA RASHID KIKWETE (KUTEULIWA):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Mipango:- Kwa kuwa Watoto wengi hasa waliozaliwa kuanzia miaka ya 1990 na kuendelea hawazijui sarafu za senti 5, 10, 20, 50 na shilingi 1:-

(a) Je, Serikali haioni ni wakati muafaka sasa kurudisha sarafu hizo kwenye mzunguko wa matumizi kwa mfano Kg 1 ya mchele kuuzwa 1892.50 au 1895.75 badala ya 1900;

(b) Kwa kuwa mada ya shilingi na senti inafundishwa katika Shule zetu hasa za msingi. Je, ni lini jambo hili litatekelezwa.

8. **MHESHIMIWA DKT. PUDENCIANA WILFRED KIKWEMBE (KAVUU):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Mipango:- Bunge lilipitisha tozo ya Kodi ya Majengo ya shilingi 10,000 kwa nyumba ya kawaida na shilingi 50,000 kwa nyumba za ghorofa lakini Manispaa na Halmashauri mbalimbali nchini zimekuwa zikitoza kodi hiyo zaidi ya kiasi hicho:-

Je, Serikali inasema nini kuhusu hali hiyo.

**WIZARA YA NISHATI:**

9. **MHESHIMIWA JUMA OTHMAN HIJA (TUMBATU):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nishati:- Kasi ya usambazaji umeme Vijijini ni kubwa lakini katika baadhi ya maeneo miundombinu inayotumika hasa nguzo hairidhishi:-

Je, Serikali inaweza kutuambia ni viwango gani *(standards)* vinavyotumika katika utafutaji wa nguzo hizo.

**10. MHESHIMIWA DAVID ERNEST SILINDE (MOMBA):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nishati:-

Je, ni lini Serikali itakamilisha miradi ya umeme katika Vijiji ambavyo havijafikiwa katika Halmashauri ya Momba.

**WIZARA YA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO:**

**11. MHESHIMIWA TASKA RESTITUTA MBOGO (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano:- Katika Uwanja wa Ndege wa Kilimanjaro ipo karakana ya kutengeneza ndege *(hangar)* ambayo ilijengwa na Serikali ya Uholanzi lakini sasa hivi haitumiki:-

(a) Je, ni lini Serikali itafufua karakana hiyo ili ndege zetu za Bombardier na nyingine ziweze kufanyiwa matengenezo hapo;

(b) Je, ni nani mmiliki wa Uwanja huo wa Ndege.

**12. MHESHIMIWA ZACHARIA PAUL ISSAAY (MBULU MJINI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano:- Wilaya ya Mbulu haina barabara ya lami kutokana na kuzungukwa na Bonde la Ufa kuanzia Karatu, Mto wa Mbu, Babati – Hanang' hivyo kufanya magari makubwa kutoka Uganda, Kenya na Dar es Salaam kuzunguka umbali mkubwa ili kufika Mbulu Mjini:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kutekeleza ahadi yake ya kuweka lami katika barabara ya Karatu – Mbulu – Hydom – Mkalama – Lalagu Shinyanga ili kurahisisha usafiri katika njia hiyo.

**WIZARA YA MALIASILI NA UTALII:**

**13. MHESHIMIWA VENANCE METHUSALAH MWAMOTO (KILOLO):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maliasili na Utalii:-

Je, ni kiasi gani cha fedha kinatolewa kwa Wilaya ambazo zinapakana au zilizo na Hifadhi za Taifa ikiwemo Wilaya ya Kilolo katika Hifadhi ya Udzungwa.

**14. MHESHIMIWA RAPHAEL JAPHARY MICHAEL (MOSHI MJINI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maliasili na Utalii:-

Je, Serikali imejipanga vipi kumaliza madai ya msingi na ya muda mrefu kwa waongoza Watalii, Wapagazi na Wapishi kutambuliwa kwa kima cha chini cha mishahara, mikataba ya kazi inayoendana na kazi zao, malipo ya posho kwa huduma wanazotoa kwa siku, Sera shirikishi katika kutatua matatizo yao na utalii wa nchi kwa ujumla na malipo ya huduma za jamii kama vile afya na majanga.

**WIZARA YA HABARI, SANAA, UTAMADUNI NA MICHEZO:**

**15. MHESHIMIWA RASHID ABDALLAH SHANGAZI (MLALO):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Habari, Sanaa, Utamaduni na Michezo:-

Je, ni lini Wilaya ya Lushoto itaanza tena kupokea matangazo ya Radio ya Taifa (TBC).

## VI. MISWADA YA SHERIA YA SERIKALI:

***(Kusomwa Mara ya Pili, Kamati ya Bunge Zima na Kusomwa Mara ya Tatu)***

Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali (Na. 5) wa Mwaka 2017 *[The Written Laws (Miscellaneous Amendments) (No. 5) Bill, 2017].*

**DODOMA** **S.N. KAGAIGAI**
**30 JANUARI, 2018** **KATIBU WA BUNGE**